BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Nne – Tarehe 12 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu kuwasilisha Ripoti ya

Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

19. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Katika utaratibu wa kawaida Watanzania wote wenye Hati za Kusafiria (Passport) hutakiwa kuzihuisha (Renew) tena hati zao hizo baada ya muda wa matumizi kumalizika (Expire Date). Hata hivyo, taratibu za kuzihuisha zinakuwa sawa na waombaji wapya, jambo ambalo huleta usumbufu kwa wenye hati hizo.

    (a) Kwa kuwa kila mwenye Hati za Kusafiria taarifa zake zote zinakuwa zipo katika Idara ya Uhamiaji, Je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea muombaji huyo kutakiwa kufuata masharti ya muombaji mpya.

    (b) Je, ni Hati ngapi za Kusafiri zimetolewa katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2022 katika Ofisi za Idara ya Uhamiaji, Zanzibar.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

31. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametangaza na ameonesha nia nzuri ya kukwamua maisha ya watu Zanzibar kupitia mikopo nafuu ya IMF ambayo haina riba kwa vikundi vya wajasiriamali na watu binafsi.

    (a) Je, agizo lake limetekelezwa kwa kiasi gani.

    (b) Je, ni wajasiriamali wangapi wamefaidika na mkopo huo hadi sasa.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

77. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na

Mipango:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa juhudi zake za kufanya tafiti mbali mbali ili kuweza kujua uhalisia wa mambo mbali mbali kwa lengo la kujiridhisha kupitia mambo hayo. Hata hivyo, matokeo ya tafiti hizo hayawafikii wananchi kwa kiwango kinachoridhisha.

(a) Je, kwa miaka mitano iliyopita (2017-2022), kuna tafiti ngapi zimeshafanyika na kukamilika.

(b) Je, tafiti hizo zililenga maeneo gani na ni njia gani zilitumika kufikisha matokeo yake kwa wananchi na wadau wengine.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

47. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa viwili vikubwa kwa maana ya Unguja na Pemba. Na kwakuwa pembezoni mwa visiwi hivi viwili vipo visiwa vyengine vidogo vidogo kama vile Tumbatu, Kojani, Makoongwe, Fundo na vyenginevyo. Na kwakuwa usafiri unaotumika katika visiwa hivi vidogo ni usafiri wa mashua na boti ndogo ndogo ambazo husafirisha abiria bila ya kufuata kanuni wala kuwa na vifaa vya uokozi na kubeba idadi yoyote ya abiria kwa kuwa hazikuwekewa utaratibu wa idadi maalum ya abiria wake.

(a) Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu maalum wa kufanya ukaguzi wa kila kipindi katika mwaka pamoja na kuvipangia vyombo hivi idadi ya abiria kwa majibu wa uwezo wa chombo husika.

(b) Kwakuwa usafiri wa baharini katika nchi yetu hauna uangalizi kama vile ulivyo usafiri wa barabarani. Na kwakuwa nchi yetu haina utaratibu wa kuwa na “Marine traffic”, Je, ni lini Serikali itaweka CCTV Camera baina ya visiwa hivi vidogo na mwambao wa visiwa vikubwa, ili kudhibiti usafiri na usafirishaji baina ya visiwa hivi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

46. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la

Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua juhudi tofauti katika kuimarisha michezo ya ndani na nje ya nchi yetu. Hata hivyo, kuna baadhi ya michezo ina uhaba mkubwa sana wa viwanja ukiwemo mchezo wa Kabadi, Golf, Tenis table na michezo mengineyo.

(a) Je, Serikali imefanya juhudi gani kutatua changamoto hiyo.

(b) Kwa kuwa Wizara yako iliahidi kulirudisha kombe la Muungano kushindaniwa hapa Zanzibar bila ya ahadi hiyo kutekelezwa hadi leo, Je, kuna kikwazo gani cha kutokutekelezwa kwa ahadi hiyo.

<u>**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**</u>

80. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya awamu ya kwanza kwa heshima kubwa iliwajengea nyumba bora za kuishi wananchi wake katika sehemu mbali mbali zikiwemo Micheweni, Michenzani, Madungu, Makunduchi na Muambe, kwa lengo la kuwapatia makazi bora wananchi wake. Hata hivyo kwa kuzingatia kuwa nyumba hizo zimekuwa za muda mrefu, yamejitokeza mashaka ya uimara na umadhubuti wa nyumba hizo.

(a) Je, Serikali imejiridhishaje juu ya umadhubuti (Life Span) wa nyumba hizo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wawekezaji ili kuona ni kwa namna gani nyumba hizo zinaweza kuboreshwa kwa lengo la kuondosha khofu ya baadae.

<u>**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**</u>

64. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali imeanza hatua za awali za kulifanyia matengenezo

Tangi la maji Safi na Salama lililopo katika jimbo la Mtambile kwa kuleta baadhi ya vifaa vyake, ingawaje muda mrefu umepita bila ya kufanyika kwa matengenezo yaliyokusudiwa. Jambo hilo linawapa wasiwasi wananchi waliokuwa wakitegemea huduma ya maji kupitia tangi hilo na kusababisha usumbufu wa upatikanaji wa huduma hiyo muhimu.

(a) Je, ni lini Serikali italifanyia matengenezo tangi hilo ili liweze kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wa eneo hilo.

(b) Je, ni sababu gani zilizopelekea hadi leo kukwama kwa matengenezo yaliyokusudiwa ya tangi hilo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

20. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika shughuli ya Utafutaji wa Nishati ya Mafuta na Gesi asilia baadhi ya nyumba na vipando viliathirika na sasa ni muda mrefu wananchi hawa hawajalipwa fidia.

Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa fidia wananchi hawa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

13. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kilimo cha “Sunflower” kinaonekana kushamiri zaidi katika maeneo yote kisiwani Pemba.

(a) Je, kuna utafiti wowote ambao Serikali imeufanya juu ya kilimo hiki visiwani mwetu. Na kama Serikali iliwahi kufanya utafiti huo ni yepi hasa yalikuwa matokeo yake.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliimarisha zao hili visiwani mwetu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

10. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali imejipanga kujenga skuli mbili, moja Unguja na moja Pemba ambazo ni maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu. Na kwa kuwa kuna changamoto kubwa ya upungufu wa walimu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye ulemavu.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa baada ya kukamilika kujengwa kwa skuli hizo, wanapatikana walimu wa kutosha kwa ajili ya kupunguza changamoto hizo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

Ripoti ya Ofisi ya Rais Ikulu kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**12 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**